# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA SABA

**07 NOVEMBA, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

# MKUTANO WA KUMI NA TATU

## KIKAO CHA SABA – TAREHE 07 NOVEMBA, 2023

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 36 la Tarehe 08 Septemba, 2023;
2. Toleo Na. 37 la Tarehe 15 Septemba, 2023;
3. Toleo Na. 38 la Tarehe 22 Septemba, 2023;
4. Toleo Na. 39 la Tarehe 29 Septemba, 2023;
5. Toleo Na. 40 la Tarehe 06 Oktoba, 2023;
6. Toleo Na. 41 la Tarehe 13 Oktoba, 2023;
7. Toleo Na. 42 la Tarehe 20 Oktoba, 2023;
8. Toleo Na. 43 la Tarehe 27 Oktoba, 2023; na
9. Toleo Na. 44 la Tarehe 03 Novemba, 2023;

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**87. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Halmashauri ya Mji Mdogo wa Tukuyu itapewa mamlaka kamili baada ya kukamilisha taratibu na kukidhi vigezo.

**88. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Kitengo cha Watoto Njiti katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi.

**89. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaboresha Vituo vya Afya vya Kinyangiri na Mkalama kwa kujenga majengo ya upasuaji na wodi.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**90. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, kuna mkakati gani wa kujenga viwanda maalum na maghala ya ubaridi kwenye eneo la Tanganyika *Packers* Mbalizi.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**91. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani kudhibiti Mto Nakasangwe na Mto Tegeta inayopanuka kwa kasi na kutishia maisha ya watu na mali.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**92. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha muundo wa Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi.

## WIZARA YA KILIMO:

**93. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwasaidia Wakulima wa Kahawa ya Arabika Tarime ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

**94. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itahakikisha mfumo wa uuzaji wa Zao la Kokoa unamnufaisha Mkulima badala ya Wafanyabiashara wachache.

**WIZARA YA UJENZI:**

**95. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itatoa fedha zote za ujenzi wa barabara ya lami Karatu – Mbulu – Haydom hadi Sibiti ili ujenzi uendelee.

**96. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Vibanda vya Wajasiriamali pembezoni mwa barabara ya njia nane Kimara hadi Kiluvya utaanza.

**97. MHESHIMIWA MWATUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani kupunguza msongamano wa maroli barabarani.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**98. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itarudisha masomo ya kazi za mikono kama useremala, mapishi, kushona, kilimo, ujenzi kwa Shule za Msingi na Sekondari.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**99. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Kata za Ruvu, Msindo, Mshewa, Vudee, Mhezi, Tae na Suji - Same zitapelekewa mawasiliano ya simu.

**100. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya mawasiliano ya simu Kata ya Masaka – Kalenga.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**101. MHESHIMIWA INNOCENT EDWARD KALOGERIS (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama za Mwanzo katika Tarafa za Bwakira, Mvuli na Matombo – Morogoro Vijijini.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**102. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itawamegea eneo Wananchi wa Visiwa vya Maisome kutoka Hifadhi ya Maisome.

**WIZARA YA FEDHA:**

**103. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kuna mpango gani wa kutenganisha malipo ya majengo kwa nyumba yenye zaidi ya mita moja ya umeme.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**104. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, maombi mangapi ya usajili wa Taasisi na Madhehebu ya Dini yamewasilishwa tangu 2016 na hazijapatiwa usajili na sababu za kutosajiliwa.

## WIZARA YA MAJI:

**105. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na mrefu wa kukarabati Mradi wa Maji wa Makonde Mkoani Mtwara.

## WIZARA YA NISHATI:

**106. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Wakandarasi wangapi kutoka Mkoa wa Kagera wamepata kazi katika mnyororo wa ujenzi wa Bomba la Mafuta la Hoima – Tanga.

## IV. KAMATI YA MIPANGO:

## WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa

unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc*** |
| **07 NOVEMBA, 2023** | **KATIBU WA BUNGE** |